



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UCHAGUZI MDOGO WA UDIWANI KATIKA
KATA SITA ZA TANZANIA BARA

Dodoma, 03 Septemba, 2021

Tume imepokea barua kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa akiitaarifu juu ya kuwepo kwa nafasi wazi za Madiwani kwenye kata sita (6) za Tanzania Bara. Nafasi hizo zilitokana na kufariki kwa Madiwani wa Kata hizo na kukosa sifa ya uraia.

Kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha Kifungu cha 13 (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume imeandaa Uchaguzi Mdogo ili kujaza nafasi za Udiwani kwenye Kata sita (6) za Tanzania Bara.

Uchaguzi huu Mdogo wa Udiwani katika Kata sita (6) utafanyika sambamba na Uchaguzi Mdogo wa Ubunge wa Majimbo mawili (2) ya Konde, Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba – Zanzibar na Ushetu, Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu Mkoa wa Shinyanga Tanzania Bara.

Kata hizo sita (6) za Tanzania Bara ni:

Na.	MKOA	HALMASHAURI	JIMBO	KATA
1.	Kigoma	Wilaya ya Kasulu	Kasulu Vijijini	Kagera Nkanda
2.	Kilimanjaro	Wilaya ya Mwanaga	Mwanaga	Kileo
3.	Mara	Wilaya ya Bunda	Bunda Vijijini	Neruma
4.	Njombe	Wilaya ya Wangin'ombe	Wanging'ombe	Luduga
5.	Rukwa	Wilaya ya Kalambo	Kalambo	Lyowa

6.	Tabora	Wilaya ya Urambo	Urambo Mashariki	Vumilia
----	--------	------------------	------------------	---------

Ratiba ya Uchaguzi Mdogo wa Kata sita (6) Tanzania Bara ni kama ifuatavyo:-

Na.	TUKI	TAREHE
1.	Wagombea kuchukua fomu za uteuzi	13 - 19 Septemba, 2021
2.	Uteuzi wa wagombea	19 Septemba, 2021
3.	Kampeni za Uchaguzi	20 Septemba - 08 Oktoba 2021
4.	Siku ya kupiga kura	09 Oktoba 2021

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaendelea kuvikumbusha vyama vya siasa na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi, taratibu, miongozo na maelekezo yatayotolewa na Tume kipindi cha uchaguzi mdogo.


Dkt. Wilson Mahera Charles

Mkurugenzi wa Uchaguzi

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI